

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**

**SHULE YA SEKONDARI HAWA MCHOPA**



**JINA LA MWANAFUNZI:** .....

**S/M:** .....

Napenda kukujulisha kuwa wewe..... wa Shule ya Msingi  
..... umechaguliwa kuijunga na masomo ya sekondari kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari  
ya Hawa Mchopa iliyopo katika wilaya ya Ruangwa,kata ya Malolo, Kijiji cha Nangumbu.  
Kwa niamba ya jumuiya ya shule ya Hawa Mchopa ninakupongeza sana kwa kuchaguliwa kwako kuijunga na shule hii.

**SHULE YA SEKONDARI HAWA MCHOPA** ni shule ya kutwa inayojengwa na wanajamii wa kata mbili za Malolo na Nanganga. Kwa kuwa shule ni ya kutwa , ni mategemeo yetu utatoka nyumbani kwako na kufika shule mapema kwa muda uliopangwa na si vinginevyo.

**UNASHAURIWA:-** Kama nyumbani kwako ni mbali sana na shule na kwamba hutaweza kufika shule kwa muda uliopangwa na shule, ni vema utafute mahali pa kuishi karibu na shule aidha iwe kwa kupangwa au kwa ndugu. Lakini shule haita mvumilia mwanafunzi atakayechelewa shulenii kwa kisingizio cha kutoka mbali.

Ni matumaini ya shule ya Hawa Mchopa kuwa hata wewe utaona ni tunu kubwa kwako kuijunga na kusoma katika shule hii, na kwamba utatumia fursa hii uliyopewa kujielimisha kwa kadri ya uwezo wako wote na nguvu zako zote na kwa akili yako yote ili upate kile taifa lichachotegemea ambacho ni ELIMU BORA.

Kwa kuwa katika ngazi hii ya elimu (Sekondari) masomo yote isipokuwa “SOMO LA KISWAHILI TU” yanafundishwa kwa kiingereza, ili basi ili usome na ufaulu vizuri inakupasa kutumia lugha ya kiingereza kwa mawasiliano muda wote na si vinginevyo, kama slogan ifuatayo inavyosema “NO ENGLISH NO COMMUNICATION”. Kwa mujibu wa kauli mbiu hii, ni makosa kwa mwanafunzi kuwasiliana kwa Kiswahili au lugha nyingine awapo katika mazingira ya shulenii.

Ukitekeleza hilo basi utakuwa kwenye mstari wa kutekeleza MOTTO wa shule usemao

“DILIGENCE AND DISCIPLINE FOR QUALITY EDUCATION”

Soma fomu yote na uelewe maelekezo yote kasha ukikubaliana na haya basi ndio ufile.

.....  
**HASSAN AHMAD MBAROUK**  
**MKUU WA SHULE**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**

**SHULE YA SEKONDARI HAWA MCHOPA**



**MAAGIZO YA AWALI YA KUJIUNGA NA SHULE MWAKA .....**

JINA .....

**A: SARE ZA SHULE**

**i) WAVULANA**

- Suruali ya kitambaa kizito ya rangi ya ugoro (Brown) iliyoshonwa vyema, isiyobana na itakayovaliwa na mkanda.
- Shati la kitambaa cheupe la mikono mifupi, lisilobana, refu na linalofaa kuchomekeea.
- Mkanda mweusi wa ngozi au plastiki, unaofunga sawasawa. NB: Ni marufuku kuvaat mkanda ya tambi.
- Viatu vyeusi vya ngozi.
- Tai rangi ya ugoro yenye mistari mweupe. (**ITAPATIKANA SHULENI TU KWA TSH. 3,000/=**)
- Tisheti (T-Shirt) ya shule ya rangi ya ugoro mpauko (**ITAPATIKANA SHULENI TU KWA TSH. 10,000/=**)
- Muhuri wa shule (**UTAPATIKANA SHULENI TU KWA TSH. 1,000/=**)
- Soksi ndefu nyeusi.
- Suti ya mazoezi (traki suti) ya rangi ya zambarau (Jezi ya Mbeya City)
- Raba za michezo na Sweta la rangi ya ugoro

**ii) WASICHANA**

- Sketi ya kitambaa kizito ya rangi ya ugoro (Brown), isiyobana ambayo inashuka kupita magotini.
- Shati jeupe la kitambaa kizito lisilobana, la mikono mifupi, pia liwe refu kiasi cha kuchomekeea.
- Tai rangi ya ugoro yenye mistari mweupe. (**ITAPATIKANA SHULENI TU KWA TSH. 3,000/=**)
- Tisheti (T-Shirt) ya shule ya rangi ya ugoro mpauko (**ITAPATIKANA SHULENI TU KWA TSH. 10,000/=**)
- Muhuri wa shule (**UTAPATIKANA SHULENI TU KWA TSH. 1,000/=**)
- Viatu vyeusi vya visigino vya kawaida.
- Sokis nyeupe ndefu (stockings)
- Suti ya mazoezi (traki suti) ya rangi ya zambarau (Jezi ya Mbeya City)
- Raba za michezo na Sweta la rangi ya ugoro

**NB: Kwa waislamu wanaotaka kuvaat HIJABU ishonwe kama ifuatavyo;**

- ❖ Suruali au sketi ndefu ya rangi ya ugoro (Brown) inayofanana na sketi.
- ❖ Blauzi (shati) jeupe, refu inayofikia magotini na iwe na mikono mirefu. (Nusu kanzu)
- ❖ Ushungi au kilemba cheupe.

**B: VIFAA VYA DARASANI**

- i) Daftari kubwa (kaunta buku) 09 au zaidi na peni za kutosha za wino wa bluu au nyeusi.
- ii) Daftari ndogo (MSOMI au KOROSHO) 9 za mazoezi.
- iii) Mkebe wa vifaa vya hisabati. (Mathematical set) pamoja na Rula ya sm 30 au au inchi
- iv) Mkoba wa kubebia daftari, ni MARUFUKU mifuko ya Rambo au kitambaa (nguo)
- v) Dictionary
- vi) Bunda moja la karatasi nyeupe (RIM Paper)

**C: MAHITAJI MENGINE**

- i) Jembe aina ya ngwamba lenye mpini. (Jembe kubwa na na si kijembe)
- ii) Panga au kwanja, (viwe vipyta na vimenolewa).
- iii) Ndoo moja
- iv) Picha nne za passport size akiwa amevaa sare ya shule na nyuma rangi ya bluu.
- v) Nakala ya cheti cha kuzaliwa na kama hana kaape mahakamani na utele Affidavity. (cheti cha kiapo cha kuzaliwa)

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**

**SHULE YA SEKONDARI HAWA MCHOPA**



**SHERIA ZA SHULE**

Kila mwanafunzi awapo shulenii atalazimika kufuata kikamilifu sheria zote za shule. Aidha mwanafunzi atalazimika kufuata maelekezo mengine yote kadri yatakavyouka yanatolewa na mamlaka ya shule.

- 1.i) Awaheshimu walimu na wafanyakazi wote waliopo shulenii kama walezi wake.
  - ii) Asimame na kumsalimia mwalimu au mtu yejote anayemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye mkutano wowote ule.
  - iii) Ampokee mzigo yoyote anayemzidi umri anapopita karibu yake.
  - iv) Aheshimu na kuthamini mali yoyote ya shule.
  - v) Akae kimya wakati wowote na aombe ruhusa anapotaka kutoka nje ya darasa kwa sababu yoyote ile.
  - vi) Anyooshe mkono juu na asimame anapouliza au kujibu swali na napoongea na mwalimu.
  - vii) Aepuke kutumia lugha chafu kwa makusudi au bahati mbaya wakati wowote kati yake na mwingine yoyote Yule. Kutumia lugha chafu au matusi ni kosa la kuadhibiwa.
  - viii) Aonyeshe heshima shulenii awapo nje na ndani ya darasa au eneo lolote lile la shule. Kugumia au kupiga kelele hakuruhusiwi.
  - ix) Si ruhusa mwanafunzi kuvuta sigara, kunywa Pombe au kutumia kilevi chochote kile kama vile madawa ya kulevy na bangi.
  - x) Aheshimu bendera ya taifa na ya chama tawala, wimbo wa taifa, nembo za taifa na pia awaheshimu viongozi wa chama na serikali.
- 2.i) Mwanafunzi anapaswa kufahamu na kutii kengele zote zinazogongwa shulenii. Aidha mwanafunzi anapaswa kutii ishara yoyote ya kuitwa na kukimbia kuelekea kule alikoitwa.
  - ii) Ahudhurie vipindi vyote vya darasani pamoa na kazi za mikono zilizopangwa katika ratiba ya shule.
  - iii) Ahudhurie mikutano yote ya shule kama vile Parade ya asubuhi, baraza la shule, kupandisha bendera, kujisomea darasani baada ya vipindi, mikutano ya darasa na bweni.
  - iv) Kufanya mitihani na majoribio yote yanayotolewa kwake.
  - v) Aonyeshe bidii darasani na kufanya mazoezi yote yatolewayo. Ni kosa la kudhibiwa kwa mwanafunzi kupata wastani wa chini ta asilimia hamsini (50%)
- 3.i) Mwanafunzi apate ruhusa ya maandishi kwa mwalimu wa zamu anapotaka kutoka nje ya eneo la shule kwa shughuli muhimu kwa masaa machache.
  - ii) Apate ruhusa ya maandishi kwa mkuu wa shule kila anaposafiri wakati wa shule nje ya eneo la shule kwa zaidi ya siku moja au anapotaka kutoka nje ya wilaya ya Ruangwa.
  - iii) Ni marufuku kwa mwanafunzi kutembelea au kuonekana katika maeneo yafuatayo bila idhini ya mamlaka ya shule;
    - ❖ Jiko la shule
    - ❖ Ofisi za shule
    - ❖ Nyumba za walimu/wafanyakazi
    - ❖ Maabara ya shule.
  - iv) Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda katika nyumba za kulala wageni (Guest houses), maeneo ya starehe, vilabu vya pombe za kienyeji, Baa, kumbi za dansi au kumbi za starehe za usiku maarufu kama DISKO.
- 4.i) Avae vazi rasmi la shule wakati wote wa masomo na wakati wa shughuli za kishule kama vile baraza la shule, midahalo na anapokuwa na ruhusa ya kutoka nje ya eneo la shule kwa shughuli yoyote ile.
  - ii) Ni mwiko kwa mwanafunzi yoyote kuongeza mapambo au marembo yoyote juu ya sare ya shule kama vile bangir, herein, shanga, kidani, rozali, tasbih, kupaka rangi za kucha, mdomo au macho, kutia dawa nywele kama curl, relaxer au wave, kurefusha rasta na kukata nyusi.
  - iii) Mwanafunzi anapaswa kuzitunza nywele kwa unadhifu na huruhusiwikunyoa kipara bila ushauri wa mwalimu au daktari, pia mitindo mbalimbali kama vile denge, panki na unga.
  - iv) Avae mavazi ya heshima yanayokubalika kwa kadiri ya mila na desturi zote.
  - v) Haruhusiwi kufuga ndevu, mustachi au sharafa.
5. Ajiepushe kabisa kufanya makosa ambayo yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule kama;
  - i) Wizi (ii) Uasherati (iii) Ulevi (iv) Kupiga/kupigana (v) Kuharibu kwa makusudi mali za shule (vi) Kudharau nembo za taifa kama wimbo wa taifa na viongozi wa chama na serikali (vii) kuoa/kuolewa (viii) Kupata/kusababisha mimba (ix) kutoa mimba (xi) kugoma, kuchochea, au kuongoza uvunjifu wa amani na usalama wa shule. (xii) kumiliki simu ya mkononi
6. Wakati wote mwanafunzi atumie akili na busara zake.
7. Ni makosa kutojua sheria za shule.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**

**SHULE YA SEKONDARI HAWA MCHOPA**



**FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE – USAJILI**

Jina: ..... Namba ya shule: .....

Jina la baba: .....

Jina la mama: .....

Dini: .....

Jinsia: Msichana/Mvulana (*Kata isiyohusika*)

Mkoa: ..... Wilaya: ..... Kijiji: .....

Kabila: ..... Tarehe ya kuzaliwa:

Anuani ya Mzazi/Mlezi: .....

Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi: .....

(*Ikiwa hukai na mzazi au mlezi andika jina na anuani yake.*)

Jina la mlezi: ..... Anuani yake: ..... Kazi yake: .....

Shule msingi uliyofania mtihani wa darasa la saba: .....

(*kama umehamia kutoka shule nyingine*)

Jina la shule ya sekondari: ..... Anuani ya shule hiyo: .....

Tarehe: ..... Sahihi ya Mzazi/Mlezi: .....

**AZIMIO LA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE**

**A: SEHEMU YA MWANAFUNZI**

1. Mimi ..... ninakubali/sikubali kijiungu na shule ya sekondari ya Hawa Mchopa katika kidato cha ..... Na nitafika shuleni bila ya kucheleva na nitafuata sheria zote za shule.
2. Anuani yangu ya kudumu ni:-  
.....  
.....

Sahihi ya mwanafunzi: ..... Tarehe: .....

**B: SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

1. Mimi ..... Nimekubali/sikubali mtoto wangu ..... ajiunge na shule ya sekondari Hawa Mchopa kuanzia tarehe ..... Na ninahaidi kumpatia vitu vyote vitakavyohitajika shuleni kama atakavyoagizwa.
2. Anuani yangu ya kudumu ni:-  
.....  
.....

Sahihi ya Mzazi/Mlezi: ..... Tarehe: .....

**NB: Njoo Na Fomu Hii Ikiwa Imejazwa Kikamilifu Siku Ya Kufungua Shule.**

.....  
HASSAN AHMAD MBAROUK  
MKUU WA SHULE

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
PRESIDENT'S OFFICE  
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT AUTHORITY



**MEDICAL CHECK-UP FORM**

Form No. 1

HAWA MCHOPA SECONDARY SCHOOL,  
P O BOX 147,  
RUANGWA  
DATE: .....  
Ref No: .....

Date: .....

TO THE MEDICAL OFFICER

.....  
.....  
.....

**PUPIL FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical officer in respect of all students from this school.

1. Pupil full name: .....
2. Age: ..... Year: ..... Sex: .....
3. Blood count (Red and White) .....
4. Stool examination .....
5. Urinalysis .....
6. Syphilis Test .....
7. Venereal disease test .....
8. T. B Test .....
9. Ear Test .....
10. Eye test .....
11. Chest .....
12. Spleen .....
13. Abdomen .....
14. Urine for plan test .....
15. Pregnancy test .....

Additional information (if any) eg. Physical defect of impairment (i.e.) arm, leg infections, chronic or family diseases etc

.....  
.....  
.....  
.....

I certify that the above student is **FIT/NOT FIT** to pursue education as stated above.

Signature: .....

Designation: .....

Station: .....

Date: .....